

Je, ninapaswa kufanya nini ikiwa nina vipele vipya au ambavyo chanzo chake hakijulikani?

HOMA YA NYANI (MONKEYPOX)

Niligundua vipele au malengelenge mapya katika mwili wangu na sina uhakika kuhusu chanzo chake, ninapaswa kufanya nini ili kujilinda na kuwalinda wengine?

WASILIANA NA MTOA HUDUMA WA AFYA

Wasiliana na mtoa huduma wako wa matibabu ya msingi ili kujadili dalili zako na kubainisha ikiwa tathmini zaidi inahitajika. Vaa barakoa wakati unapokea huduma. Ikiwa huwezi kumtembelea mtoa huduma wako wa matibabu ya msingi mara moja au huna mtoa huduma, zingatia machaguo haya ya matibabu:

- Huduma za tiba kupitia vifaa vya mawasiliano
- Vituo vya Matibabu ya Haraka
- Kliniki ya Virusi vya Ukimwi/Magonjwa ya Zinaa (HIV/STI) ya Forest Community Health Center-jinsi upatikanaji unavyoruhusu

Hakikisha kwamba unamwambia mtoa huduma wako wa afya ikiwa umekuwa na mgusano na mtu ambaye ana homa ya nyani inayowezezana au iliyothibitishwa au ulikuwa katika eneo ambapo homa ya nyani imeripotiwa.

WALINDE WENGINE

Hadi baada ya kuhudumiwa na mtoa huduma wa afya na amebainisha chanzo cha vipele au malengelenge, epuka mgusano wa karibu wa ngozi kwa ngozi na wengine, ikiwa ni pamoja na ngono au kufanya mapenzi na mtu yeyote, ili kuepuka maenezi zaidi.

JE, NAPASWA KUFUATILIA NINI?

Vipele vya homa ya nyani vinaweza kuonekana kama chunusi au malengelenge ambayo huonekana kwenye uso, ndani ya mdomo, katika sehemu nyingine za mwili, kama mikono, miguu, kifua, viungo vya uzazi au mkundu. Mifano ya picha ya vipele vya Homa ya Nyani:



Hatari kwa umma ni ndogo kwa ujumla, hata hivyo, mtu yeyote ambaye amekuwa na mgusano wa karibu na mtu ambaye ana homa ya nyani anaweza kupata ugonjwa huo, bila kujali jinsia au mwelekeo wa kimapenzi. Hadi kufikia sasa, kesi nyingi zimekuwa kwa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume (MSM), lakini kila mtu anapaswa kuchukua tahadhari ili kuzuia maambukizi.

Utambuzi wa umiliki wa picha: CDC